



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASASI



Simu: 023 – 2510013,2510031
Halmashauri ya Wilaya
Nukushi; +023 – 2510031
Barua pepe: ded@masasidc.go.tz
Tovuti: <http://www.masasidc.go.tz>

S.L.P 60
Masasi
Mtwara
TANZANIA

Kumb. Na. MDC/L. 10/2/VOL X/27

Tarehe: 04/03/2023

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi amepokea kibali cha Ajira Mbadala kutoka kwa Katibu Mkuu OR - Utumishi chenye kumbu Na. **FA.170/362/01”B”/57** cha tarehe **10/01/2023**. Hivyo napenda kuwatangazia wataanzania wote wenye sifa kutuma maombi kwa nafasi tatu (3) za Mtendaji wa Kijiji daraja la III kwa kuzingatia sifa zifuatazo:-

1.0 SIFA ZA MWOMBAJI (MTENDAJI KIJIKI DARAJA LA III – NAFASI 03)

1. Awe na Elimu ya kidato cha nne (IV) au cha sita (VI)
2. Awe amefuzu mafunzo ya Astashahada (NTA - level 5) katika moja ya fani zifuatazo;- Utawala, Sheria, Maendeleo ya jamii, Usimamizi wa Fedha na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo - Dodoma au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

2.0 KAZI NA MAJUKUMU

1. Afisa masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
2. Kusimamia ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika Kijiji.
3. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika Kijiji.
4. Kuwa Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
5. Kutafsiri na kusimamia sera, sheria na taratibu.
6. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika Eneo Lake.

7. Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kamati za kitaalam katika kijiji.
8. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji.
9. Kusikiliza, kupokea na kutatua malalamiko na migogogro ya wananchi.
10. Kusimamia utungaji wa sheria ndogondogo za kijiji.

3.0 NGAZI YA MSHAHARA

Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali – **TGS B₁**

4.0 MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

- i. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45.
- ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa
- iii. Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi (CV) yenye anuani na namba zao za Simu na Majina mawili ya wadhamini.
- iv. Maombi yaambatishwe pamoja na nakala za vyeti vya Taaluma
- v. Maombi yote yaambatishwe na picha mbili 2 za passport size za hivi karibuni na ziandikwe majina kwa nyuma
- vi. Waombaji waliosoma nje ya nchi waaambatanishe cheti cha ulinganifu (Equivalent Certificate) kutoka Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA) au kwenye mamlaka husika.
- vii. Waombaji wenye vyeti vya ngazi ya NTA Level 4 (Basic technician Certificate) maombi yao hayatafanyiwa kazi. Cheti kinachopokelewa na kufanyiwa kazi ni NTA Level 5 (Technician Certificate).
- viii. Watakapo chaguliwa kufanya usaili watajulishwa kupitia Tovuti ya Halmshauri ambayo ni www.masasidc.go.tz
- ix. Maombi yatapokelewa kuanzia tarehe 06/03/2023 hadi tarehe 20/03/2023
- x. Maombi yatapokelewa kuanzia Tarehe Hadi Tarehe
- xi. Waombaji wote wawe na Namba ya Utambulisho wa Taifa (NIN) kutoka NIDA
- xii. Maombi yatumwe Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kwa anuani ifuatayo:-

MKURUGENZI MTENDAJI (H/W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASASI
S.L.P 60
MASASI

Tangazo hili limetolewa na;



Masumbuko B. Mtesigwa
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (M)
MASASI.

KAIMU MKURUGENZI
HALMASHAURI YA WILAYA
S. L. P. 60, MASASI

NAKALA: Katibu
Ofisi Rais,
Secretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma
S.L.P 2320
DODOMA